

**OFISI YA RAIS - TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (OR
TAMISEMI)**

SHULE YA SEKONDARI NYIHARA
S. L. P 1377
MUSOMA

13 / 12 / 2020

KUMB. Na. NYHRSS/ JOIN/ FI/ 2021

MWANAFUNZI

**YAH; KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA SHULE YA KUTWA
YA NYIHARA SEKONDARI KWA MWAKA 2021.**

Tafadhali rejea mada tajwa hapo juu. Napenda kukutaarifu kwamba, umechaguliwa kujiunga na shule yetu ya Nyihara Sekondari kwa mwaka wa masomo 2021. Shule ya Sekondari Nyihara inapatikana katika kata ya Kyang'ombe, tarafa ya Suba, kijiji cha Nyihara. Hivyo, kwa barua hii, unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 11/01/2021 (Siku ya kufungua shule). Mwisho wa kuripoti ni tar. 25/01/2021. Hata hivyo, unapaswa kuripoti shuleni ukiwa na mambo yafuatayo;

1. SARE ZA SHULE

- Shati mbili nyeupe (Tomato) za mikono mifupi kwa wasichana na wavulana
- Tai moja rangi ya damu ya mzee na moja rangi ya kijivu..
- Suruali moja rangi ya damu ya mzee na moja ya kijivu zenye marinda kiunoni na tanapu na isiwe ya kubana. Hii ni kwa wavulana.
- Sketi moja rangi ya damu ya mzee na moja kijivu zenye urefu unaofika miguuni (Kitambaa kisionyeshe viungo vya mwili wala nguo za ndani)
- Soksi jozi mbili nyeupe kwa wasichana na nyeusi jozi mbili kwa wavulana.
- Viatu vyeusi jozi mbili vya kamba visivyo na kisigino kirefu wala kuchongoka mbele. Hii ni kwa wavulana na wasichana.
- T-shirt moja ya bluu yenye kola.
- Vifaa vya michezo: Awe na viatu vya michezo jozi moja na soksi zake kwa wavulana na viatu vya raba na soksi zake kwa wasichana pamoja na track suit moja bluu kwa wote.

2. VIFAA VYA KUJIFUNZIA

- ❖ Aje na counter 10 za kuandikia nukuu (Isiwe chini ya quire 2)
- ❖ Madaftari madogo 09 kwa ajili ya mzaoezi pamoja na English course.
- ❖ Kamusi ya kiingereza (English Dictionary).
- ❖ Kalamu za wino na za mkaa kwa ajili ya kuandikia na kuchorea.
- ❖ Bado moja ya limu pepa kwaajili ya mitihani na mazoezi mbalimbali.

3. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, kwa kuzingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu na mafunzo ya ufundi yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu. Hivyo ukiwa kama mwanafunzi wa shule hii, unatakiwa kufuata maelekezo yafuatayo;

- i) Unapaswa kuripoti shule, muda wa saa 1:00 ASUBUHI kila siku za masomo.
- ii) Kuvaa sare za shule kwa wakati wote unapotakiwa.
- iii) Kuheshimu viongozi, walimu, wafanyakazi wengine, wazazi, viranja, wanafunzi wenzako na jamii kwa ujumla.
- iv) Kushiriki shughuli mbalimbali za shule, ikiwa pamoja na zile utakazopangiwa na walimu pamoja na viongozi wako.
- v) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
- vi) Kuzingatia ratiba ya shule kama inavyoelekeza.
- vii) Kutunza mali ya umma.
- viii) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani ya mipaka hiyo wakati wote uwapo shuleni.
- ix) Huruhusiwi kuwa na simu katika eneo la shule.

MUHIMU: Makosa yafuatayo yanaweza kukusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule;


- i) Kuwa mjamzito/ Kupata mimba
- ii) Kutoa mimba
- iii) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
- iv) Kukataa adhabu kwa makusudi.
- v) Kudharau Bendera ya Taifa.
- vi) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- vii) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile bangi, mirungi, kuberi n.k
- viii) Ubakaji
- ix) Uasherati na ushoga
- x) Wizi
- xi) Kupigana au kupiga.

TANBIHI: Hakikisha unaporipoti shule siku ya kwanza, unafika na vitu vifuatavyo:

- i) Medical examination form ambayo imejazwa na mganga mkuu wa **hospitali ya serikali na si vinginevyo.**
- ii) Kivuli cha cheti cha kuzaliwa

Hongera sana, *

VICTOR PAUL KIHAGA.



THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRESIDENT'S OFFICE – REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
NYIHAA SECONDARY STUDENT'S FORM FOR MEDICAL EXAMINATION

Student's full name.....

Age

I kindly request you to examine him/her physically and mentally if he/she is fit or unfit to pursue O-level studies in our school.

Blood-count

Urine

Stool

Venereal – diseases

T. B

Ears

Eyes

Spleen

Chest

ADDITIONAL INFORMATION:

If any E.g, physical defects (arm or leg impairments, chronic or family diseases) ect

I certify that he/she is fit/unfit to persue education as stated

Name

Signature

Station

Designation

Date

Official stamp.....